# STANDARD 8 MID TERM 2 EXAM 2019

## KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nambari 1 hadi 15 zilizoachwa wazi. Kwa kila nafasi, jaza kwa jibu sahihi.***

____1____ nusu ya idadi ya watu ____2____ jamii ____3____ aina ya chakula ____4____. Wengi hula ____5____ wajaze tumbo kwa sababu ____6____ njaa. Lishe ni dawa inayoweza kuzuia maradhi fulani ____7____ mtu au dawa ___8____ kuenea kwa maradhi fulani ____9____ kuponya.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Nusura | Takribani | Nadra | Kama |
| 2. | katika | miongoni mwa | humu | kwa |
| 3. | hujali | inajali | wanajali | hawajali |
| 4. | wakulacho | ikulacho | walacho | kiliwacho |
| 5. | kwani | hili | na nia | bora |
| 6. | wamesikia | wameona | wamepata | wamehisia |
| 7. | kumwandama | yasimwandame | kuandamana | kuandama |
| 8. | inayothibiti | inayodhibiti | inayosaidia | unayopunguza |
| 9. | na | kwa | licha ya | mathalani |

Vituko vya mumewe alikuwa ____10____. ____11____ mara moja au mbili aliambukizwa maradhi ya ____12____. Nafuu hakupata maradhi yasiyo na tiba ____13____ Kumwuliza mumewe, ____14____ ni matusi na pigo ambalo hajawahi kulipata ____15____ azaliwe.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | akivifumbia macho | avikazia macho | akivitupia macho | avikodolea macho |
| 11. | Ni | Na | Si | Ja |
| 12. | kuambukiza | zinaa | mitambo | siri |
| 13. | ; | . | ? | ! |
| 14. | alichofaidi | aliyefaidi | kilichofaidi | waliyofaidi |
| 15. | jinsi | tangu | hadi | pindi |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

16. Tambua kundi la sauti sighuna **pekee**.
   A. p, b, t
   B. ch, f, dh
   C. j, g, gh
   D. dh, y, w

17. Chombo ni zana ya kazi ilhali shombo ni
   A. kifaa maalum cha kufanyia kazi.
   B. samaki wengi pamoja.
   C. harufu ya samaki aliyevuliwa.
   D. aina ya pambo la miguuni.

18. Ni sentensi gani ya kutoa amri?
   A. Kuwasili kwetu kuliwafurahisha.
   B. Ongeza bidii usije ukapatwa.
   C. Ondokeni karibu nami!
   D. Duka likamilikapo mtahama.

19. Mbele ya hakimu, alishtakiwa **<u>kulingana na</u>** sheria
   "**<u>Kulingana na</u>**" katika sentensi hii ni
   A. kihusishi
   B. kiunganishi
   C. kielezi
   D. kihisishi

20. Kanusha sentensi ifuatayo:
   **Yeye akija umwambie.**
   A. Yeye akija usimwambie.
   B. Yeye asipokuja usimwambie
   C. Wao wasipokuja usiwaambie
   D. Yeye asipokuja wala usimwambie

21. Uakifishaji **usiofaa** ni upi?
A. Timu tatu zimewasili uwanjani: Simba, Mafuta na Kamata.
B. Nora:(kwa ukakamavu) Mimi sitaki ujinga!
C. Kumbe mtu yule alikuwa jizi!
D. Mama aliniambia, Mweledi, amka ukimbie uende shuleni.

22. Chagua maendelezo **yasiyofaa.**
A. Ghilibu B. Geli
C. Gorofa D. Swala

23. Chagua sentensi inayoonyesha hali ya masharti.
A. Nitafika kesho asubuhi.
B. Ukimwona, mpe salamu zangu.
C. Wanafunzi wanasoma.
D. Kilichopotea ni changu.

24. Kipi ni kinyume cha
**Ajuza aliketi darini akalia**
A. Shaibu alisimama sakafuni akacheka.
B. Kijana alisimama sakafuni akacheka.
C. Shaibu aliketi darini akacheka.
D. Kijana aliketi darini akalia.

25. Chagua usemi wa taarifa
**"Kesho wataondoka saa ngapi?" Farida aliuliza.**
A. Farida aliomba kujua siku iliyofuata wataondoka saa ngapi.
B. Farida alitaka kujua siku iliyofuata wangeondoka saa ngapi.
C. Farida aliomba kufahamu kesho wataondoka saa ngapi.
D. Farida aliomba kujua kesho wangeondoka saa ngapi.

26. Chagua sentensi ambayo ina kivumishi tofauti
A. Mtoto yeyote ataibiwa.
B. Magari machafu hayafai.
C. Punda mwenye mkia mfupi amekufa.
D. Vitabu vingine vimenunuliwa.

27. Tegua kitendawili.
Nikimpiga mwanangu watu hucheza.
A. Ngoma B. Muziki
C. Mvua D. Shoka

28. Gharama ni pesa zinazohitajika kwa nia ya kupata huduma fulani ilhali karama ni
A. bidii alizo nazo mtu
B. sherehe fulani
C. kiongozi wa kundi
D. kipawa alicho nacho mtu

29. Chagua jozi **isiyofaa**
A. Kichunguu - mchwa
B. Kasri - malkia
C. Kiota - kasuku
D. Utandu - buibui

30. **Ndege mkubwa yu mtini**. Katika sentensi hii, kitenzi ni
A. mtini B. mkubwa
C. ndege D. yu

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Mwafrika hujulikana kwa sifa kubwa zaidi kuliko ukarimu. Ukarimu huu huonyeshwa kwa jinsi amkaribishavyo mgeni. Ni furaha kubwa mgeni kukaribishwa kiamboni wakati wowote, na hali yoyote , awe ametoa taarifa mapema au la. Hii **ni kinyume na wenzetu** katika nchi za ughaibuni.

Pindi mgeni afikapo nyumbani, tabasamu na maneno kama "karibu, chondechonde na starehe" hurutubisha imani katika mioyo ya wenyeji wake. Kongowea, mapokezi ya mikono miwili, ni dhahiri. Mara tu baada ya kuingia nyumbani, wenyeji wake hushughulika kwa matayarisho kama malazi na chakula iwapo mgeni huyo ni wa mbali. Furaha hutanda tangu makaribisho yake hadi siku ya kuaga, " kwa heri!"

Wapo wageni wa aina mbalimbali. Kunazo aina tatu kuu. Daraja la kwanza ni wale wageni ambao huwa tunaawandikia barua za makaribisho maalumu. Hawa ni ndugu au marafiki ambao hatuonani kwa muda mrefu, hivyo sisi huwaomba kutuzuru wapatapo nafasi. Kundi la pili ni la jamaa zetu. Hawa huweza kutufikia kwa makaribisho kutegemea uamuzi wao. Jamaa hao hutoa taarifa ndefu au fupi kabla ya kuanza safari ili wakirudi nyumbani wasipate mambo yameenda segemnege. Kundi la tatu hutokea ghafla hata bila taarifa yoyote.

Wakati mwingine mgeni huleta usumbufu nyumbani hasa tuwapokeapo wageni ambao hawategemewi. Hii huathiri hasa mpango wa matumizi ambao unapoingiliwa huleta shida kubwa. Jambo hili si mno kuonekana vijijini, lakini kwa wale wenye **mastakimu** yao mijini, ugeni wa aina hii huleta hekaheka nyumbani. Yapo mambo kadhaa yasababishayo wasiwasi huu. Jambo lililo wazi ni chakula. Ikiwa jamaa amepanga matumizi ya yeye , bibi yake na watoto wawili, mgeni bila shaka huongeza vinywa kuwa vitano na kutibua mipango yote ya nyumbani. Shida hii huwa maradufu iwapo mgeni huamua kukaa kwa muda wa **siku ayami.**

Wajibu wa jamaa na marafiki waamuapo kwenda mijini ugenini kuwa ingewabidi kujulisha wenyeji wao na kungojea makaribisho kabla ya kuanza safari.

---

**31.** Sifa kuu ya mwafrika kulingana na mwandishi ni
A. makaribisho
B. kiafrika
C. furaha
D. ukarimu

**32.** "**... ni kinyume cha wenzetu**..." Maana halisi ya kauli hii ni kuwa
A. waafrika hutuma taarifa kabla ya kuwatembelea wenzao.
B. wazungu hutuma taarifa kabla ya kuwatembelea wenzao.
C. ni lazima mgeni atume taarifa kabla ya kumtembelea mwenyeji.
D. waafrika hawana utamaduni.

**33.** Makaribisho kwa moyo mkunjufu katika kifungu hiki mwandishi anayaita
A. virutubisho
B. chondechonde
C. starehe
D. kongowea

**34.** Kulingana na kifungu ulichosoma, malazi na chakula huwafaa wageni
A. jamaa za wenyeji.
B. wa kutoka shambani.
C. wa mbali wasio na nia ya kurudi siku hiyo.
D. walio na ugeni wa siku nyingi.

**35.** Marafiki ambao hufika kwa wenyeji wao baada ya ombi
A. ni wale ambao hawaonani na wao kwa muda mrefu.
B. ni wale ambao hawana shughuli nyingi.
C. hupata nafasi ya kuwatembelea wenzao.
D. hawana maadili.

**36.** Jamaa anapomtembelea mwenyeji, ana hiari ya
A. kutuma taarifa.
B. kutotuma taarifa.
C. kuzuru wakati wowote.
D. kufanya apendavyo.

**37.** Ugeni ambao huvuruga makadirio ya matumizi ya nyumbani , mara nyingi ni ule wa
A. vijijini
B. mijini
C. jamaa
D. kutuma taarifa kwanza

**38.** Kinywa cha tano ambacho mwandishi anakitaja katika kifungu hiki ni kile cha
A. watoto
B. bibi
C. mgeni
D. baba

**39.** Katika aya ya mwisho mwandishi ana maoni kuwa
A. bila makaribisho wageni wasianze safari.
B. safari ianze kabla ya kuanza makaribisho.
C. ni vyema iwapo tutatuma taarifa, kisha safari ianze.
D. kumtembelea mwenyeji kusiwe na kizuizi.

**40.** **Siku ayami** ni siku
A. moja
B. chache
C. nyingi
D. haba

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Kabaka alikuwa ameketi kwake uani akisikiliza redio. Alipenda redio kama mboni ya jicho lake. Alipenda kusikiliza taarifa ya habari, matangazo ya mpira na matangazo ya kibiashara; sikwambii vipindi vya salamu. Leo ni Jumamosi majira ya jioni. Mechi kuu inachezwa kule Uingereza. Timu ya Manchester United na Arsenal zinautesa uga wa Emirates. **Yamkini** mtangazaji hakuwa kwenye uwanja wa Emirates nchini Uingereza. Lazima alikuwa katika studio Nairobi akitazama mchezo huo kwenye runinga na kuitangaza sawia kwa faida ya wasikilizaji wa redio. Mwanawe, Zawadi, aliyeshabikia Arsenal lazima anautazama mpambano huu wa mpira mahali fulani, katika ukumbi fulani jijini Mombasa anakofanya kazi hotelini.

"Lo! Jinsi dunia ilivyo ndogo siku hizi," aliwaza. Mpira unachezwa kwenye uwanja katika bara jingine wakati huo huo mawimbi yanarusha picha na sauti hadi kwenye viwambo vya runinga katika pembe mbalimbali za dunia. Isitoshe, matukio ya viwanjani yanawasilishwa kwa matangazo ya redio hadi kumfikia Kabaka kwenye kijiji chake cha Pendaraha.

Dunia imekuwa kijiji cha kweli kwa vile tukio mahali pa mbali linaweza kuathiri maeneo mengine. Labda ni maendeleo haya ya teknolojia yaliyowasababisha wanakijiji cha Pendaraha kuanza kushabikia timu za mpira za Ulaya. Walizitupa kapuni timu zao za kijijini na nchini kwa jumla. Kituo cha redio kilichokuwa kikitangaza mpira wa ligi kuu ya Uingereza kilielewa fika hilo. Wananchi wa nchi hii wameanza polepole kupenda mambo ya wengine. Wanaenzi vitu vya watu wengine . Wanapenda wanamichezo, wanamuziki, wanasiaisa na waandishi wa mataifa ya mbali.

"Sisi ni watu tunaopenda kujichukia", Kabaka akazungumza na nafsi yake. Mke wake, Pendo, ndiye aliyemzindua kutoka kataka ndoto ya mchana. Mtangazaji wa mpira aliendelea hadi mwisho wa mechi lakini ajabu ni kuwa Kabaka hakujua matokeo yake wala kipenga kilipopulizwa kuitamatisha mechi hiyo.

Wakati wa taarifa ukafika . Taarifa zilizopewa kipaumbele ni kuhusu kimbunga kilichotokea kule Ulaya na kuwaangamiza waja bila kusahau uharibufu wa mali . Deno aliyekuwa tegemeo la wazazi wake wazee alikuwa miongoni mwa waliomezwa na kimbunga hicho. Kifo cha Deno kilitangazwa kote kijijini. Wengi walihuzunika na kuomboleza mwana wao.

**41.** Kulingana na mwandishi, nia ya Kabaka kutulia pale uani siku hiyo ilikuwa ni
A. kusikiliza taarifa.
B. kusikiliza matangazo.
C. kuwatazama wapita njia.
D. kusikiliza matangazo ya mpira.

**42.** Mtangazaji wa mechi iliyotajwa kwenye kifungu hiki alikuwa
A. uwanjani Emirates B. katika redio
C. jijini Nairobi D. katika televisheni

**43.** Kabaka na mwanawe wanashabihiana kwa kuwa wote
A. ni wapenzi wa soka.
B .wanausikiliza mchezo.
C. wanautazama mchuano.
D. wanapenda sana matangazo.

**44.** Ni nani aliyefurahia sauti na picha za mchezo uliotajwa kwenye kifungu?
A. Kabaka B. Zawadi
C. Mkewe Kabaka D. Deno

**45.** Kulingana na aya ya pili ni nini ambacho kilimshangaza Kabaka?
A. Udogo wa dunia.
B. Maendeleo katika teknolojia.
C. Maendeleo katika utangazaji.
D. Dunia kuwa kitongoji.

**46.** Kabaka analaumu teknolojia kwa kuwa
A. imeifanya dunia kijiji kidogo
B. inafanikisha matangazo
C. imechangia wengi kuthamini mambo ya kigeni
D. wengi wamekuwa watumwa

**47.** Udhaifu wa Kabaka na wenzake wa kuzidharau timu za humu nchini ulitoa fursa kwa vituo vya utangazaji
A. kuanzisha matangazo kutoka ng'ambo.
B. kuwaburudisha wana soka nchini.
C. kuwapata mashabiki wa soka nchini.
D. kutangaza mechi za humu nchini.

**48.** Methali ambayo inawafaa Kabaka , Zawadi na wenzao ni
A. asiyekuwepo na lake halipo.
B. sumu ya neno ni neno.
C. kiendacho kwa mganga hakirudi.
D. mwacha mila ni mtumwa.

**49.** Kwa mujibu wa Kabaka, timu iliyoshinda mchuano aliousikiliza katika redio ilikuwa ni
A. Arsenal
B. hana habari
C. Manchester United
D. mechi ilikuwa tasa

**50.** Maana ya neno **"Yamkini"** jinsi lilivyotumika kwenye kifungu ni
A. ni kweli kuwa.
B. ni wazi.
C. haiwezekani.
D. yawezekana.



Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com